



BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA

S.L.P 38093, Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 2128691, Nukushi: +255 2128692

Barua pepe: twlbwrs@gmail.com, Tovuti: www.wrs.go.tz

Kumb Na: BA.32/292/01"1"/48

Tar: 2 Aprili, 2017

KIPINDI CHA KUOMBA LESENI ZA, MWEENDESHA GHALA NA WAKAGUZI WA GHALA MSIMU 2017/18

Bodi ya Leseni za Ghala Tanzania iliyoanzishwa kwa Sheria Na 10 ya Mwaka 2005 na Maekebisho yake Sheria Na 3 ya Mwaka 2015, Kanuni za Stakabadhi za Ghala 2017 na Taratibu zilizowekwa Serikali. Bodi imepewa jukumu la kusimamia Mfumo wa Stakabadhi za ghala nchini. Kupitia tangazo hili, wadau wote wa mazao ya kilimo ambao wanapenda kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala mnataarifiwa kuwa kipindi cha maombi ya leseni ni kuanzia tarehe 1 April, 2017 hadi 30 Augusti, 2018.

Kwa sasa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala inatoa leseni kwa kazi hizi kwa mazao ya Kahawa, Korosho, Alizeti, Ufuta, Mpunga, Mahindi, na Mbaazi.

Waombaji wote wanatakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zote kama zilivyoainishwa kwenye fomu namba 1 na 5 ambazo zinatumiwa katika mchakato wa Maombi ya leseni. Aidha, kwa kampuni mpya Wakurugenzi na wafanyakazi wapya ni lazima wahudhurie mafunzo kabla ya leseni haijatolewa.

Fomu za maombi zinapatikana katika tovuti ya Bodi <http://www.wrs.go.tz> Na mnakumbushwa kuwa maombi yote baada ya msimu yataambatana na ada ya maombi ya leseni kutoka shilingi 20,000.00 hadi 1,500,000.00 kwa kila ghala.

Mfumo wa Stakabadhi za ghala unarasimisha masoko ya mazao ya **WAKULIMA** na **WASINDIKAJI WA MAZAO YA KILIMO**.

Imetolewa na:

**AUGUSTINO W. MBULUMI
MKURUGENZI MTENDAJI**